**MASHARTI NA VIGEZO VYA JUMLA KWA WATEJA KAMPENI YA TISHA NA TEMBOCARD 2025 – TEMBOCARD NI SHWAA**

Katika masharti na vigezo hivi, maneno yafuatayo yatakuwa na maana ifuatayo:

- **“Akaunti”** inamaanisha akaunti iliyoanzishwa kwa ombi la mteja kulingana na mahitaji ya benki na sheria husika.
- **“Mmiliki wa Kadi”** inamaanisha mtu ambaye amepewa TemboCard.
- **“Mteja”** inamaanisha mtu binafsi mwenye akaunti katika benki na hivyo kuwa mmiliki wa TemboCard Visa.
- **“Punguzo”** inamaanisha upunguzaji wa gharama ya kawaida ya kitu fulani, iwe ni bidhaa au huduma.
- **“Motisha”** inamaanisha kitu kinachomhamasisha au kumtia moyo mtu kufanya jambo fulani, kwa muktadha huu ikimaanisha punguzo au marejesho ya pesa (Cashback) ili kuwahamasisha wateja kutumia kadi zao zaidi.
- **“Mfanyabiashara”** inamaanisha duka lolote linalokubali malipo kwa kutumia TemboCard kwa ajili ya bidhaa na huduma.
- **“Mpango”** inamaanisha mtandao wa kadi ambapo kadi za CRDB hutolewa chini ya Visa, MasterCard, au UPI.
- **“TemboCard”** inamaanisha aina zote za kadi za kielektroniki zinazotolewa na Benki kwa ombi la mteja kwa ajili ya huduma zinazotolewa na Benki, ambazo zinaweza kutumika kwenye POS, mtandaoni au ATM kwa ajili ya manunuzi na/au kutoa pesa taslimu.
- **“Benki”** inamaanisha CRDB Bank PLC.

**A. Masharti na Vigezo vya Jumla**

1. Kampeni hii inalenga tu wateja waliopo na TemboCard Visa (Prepaid, Credit, Debit).
2. Wafanyakazi wote wa CRDB hawatahusika katika kampeni hii ya kadi kwa wateja.
3. Aina za miamala inayohusika ni miamala yote ya ununuzi (POS na e-commerce/mtandaoni).
4. Miamala inayohusika ni ya ndani ya nchi na ya kimataifa.
5. Benki itakuwa na haki ya kutangaza kuhusu zawadi kupitia njia zake au vyombo vya habari vingine.

6. Mteja ataruhusiwa kushinda zawadi katika kundi moja tu kwa kipindi chote cha kampeni.
7. Washindi watachaguliwa kulingana na idadi ya miamala, ambapo wateja walio na miamala zaidi ya 30 kwa mwezi wataingizwa kwenye droo na mshindi atachaguliwa kwa misingi hiyo.
8. Mteja anapaswa kuwa ndani ya nchi ili kupokea zawadi yake, isipokuwa kwa makubaliano maalum. Hakuna zawadi zitakazotumwa nje ya nchi.
9. Ikiwa mshindi hatapatikana, hataki kupokea zawadi au hataki kuhusika katika matangazo ya vyombo vya habari, droo itafanywa tena ili kumpata mshindi mpya.
10. Mshindi atajulishwa kwa kupigiwa simu mara tatu kabla ya kuchaguliwa mshindi mwingine.
11. Kushindwa kutoa nyaraka muhimu, kama pasipoti kwa washindi wa safari za nje, kutasababisha kuchaguliwa mshindi mwingine.
12. Mshindi wa zawadi ya safari anatakiwa kusafiri katika tarehe iliyopangwa na benki. Kushindwa kufanya hivyo kutasababisha kuchaguliwa mshindi mwingine bila fidia yoyote.
13. Mshindi wa zawadi kuu (gari) anatakiwa kulihifadhi gari hilo (ambalo linaweza kuwa na chapa ya benki) kwa angalau mwaka mmoja kabla ya kuliuza.
14. Mshindi wa zawadi kuu (gari) atapewa bima ya kina ya gari kwa kipindi cha mwaka mmoja.

**Masharti Maalum kwa Kila Kategoria ya Kampeni**

**B. Masharti Maalum**

1. Kampeni itaendelea kwa miezi mitatu kuanzia tarehe 13 Februari 2025 hadi Juni 2025, ikiwa na zawadi za kati na zawadi kubwa.
2. Wateja wenye miamala angalau 30 kwa mwezi watahitimu kuingia kwenye droo.
3. Mshindi wa mwezi Machi atapewa safari ya kulipiwa kikamilifu kwenda Serengeti, itakayofanyika wiki ya kwanza ya Aprili.
4. Mshindi wa mwezi Aprili atapewa safari ya kulipiwa kikamilifu kwenda Serengeti, itakayofanyika wiki ya kwanza ya Mei.
5. Mshindi wa mwezi Mei atapewa safari ya kulipiwa kikamilifu kwenda Ulaya, itakayofanyika wiki ya kwanza ya Juni.

6. Mshindi wa jumla wa kampeni atashinda **gari jipya aina ya Ford Ranger**, zawadi ambayo itatolewa mwezi Julai.

**C. Ulinzi wa Taarifa Binafsi**

1. Benki itakusanya taarifa zako binafsi pale utakapo omba kutumia huduma hii ya kibenki. Taarifa hizo zitajumuisha, majina yako, anuani na namba yako ya simu, taarifa za utambuisho, taarifa na kumbukumbuku za kifedha. Taarifa hizi zitatumika kuthibitisha utambulisho wako, kutimiza kanuni na matakwa ya kisheria na kuwezesha mawasiliano mahususi kuhusiana na akaunti yako/zako, miamala ya kibenki na taarifa zote muhimu. Benki inalinda na kutunza taarifa zako binafsi kwa mifumo thabiti ili kutunza usiri wa taarifa zako binafsi na kutimiza weledi wa kibenki. Pia Benki itatunza na kubakia na taarifa zako binafsi ili kutimiza lengo liliokusudiwa tu.

2. Kwa kukubali vigezo na masharti haya, unakubali kutoa ridhaa yako kwa Benki kukusanya, kutumia na kutoa taarifa zako binafsi pale zinapohitajika watoa huduma wa Benki, Wabia wa Benki, Mamlaka za usimamizi wa mabenki na taasisi za kifedha kwa lengo la kukuhudumia, kusimamia na kuboresha huduma za kibenki. Pia Benki inaweza kutoa taarifa zako binafsi kwa mujibu wa sheria au amri ya Mahakama. Benki inakuhakikishia kwamba watakaopewa taarifa zako binafsi watawajibika kuhifadhi taarifa zako kwa usiri na kwa mujibu wa mkataba wa kuhifadhi taarifa. Taarifa zako binafsi zitatumika kwa lengo lilokusudiwa na kwa mujibu wa kanuni na sheria za nchi.

3. Una haki ya kupata taarifa zako binafsi, kurekebisha, kufuta au kuweka kizuizi au pingamizi la kutotumika kwa taarifa zako binafsi.